BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thalathini na Moja – Tarehe 22 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Kuweka Masharti Yanayohusika na Huduma za Miundombinu ya Tehama na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Kuweka Masharti Yanayohusika na Huduma za Miundombinu ya Tehama na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

237. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika Kware iliyoko Makaani, katika kijiji cha Vitongoji Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba, kumekuwa na ongezeko kubwa la mashine za kusaga kokoto (crushers). Maeneo hayo yanatumiwa na wananchi wanyonge na walipa kodi wa nchi hii kwa ajili ya kilimo na mifugo yao na hivyo huondoshwa bila ya kulipwa chochote katika ardhi hizo ambazo zimewasaidia kusukuma maisha yao kwa kipindi kirefu.

(a) Je, Serikali kwa kiasi gani inalitambua jambo hilo.

(b) Je, Serikali itawasaidia vipi wanyonge hao kuepukana na unyanyasaji huo unaofanywa na matajiri.

(c) Je, vitendo hivyo vya matajiri dhidi ya wanyonge katika maeneo hayo, havipingani na malengo ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kujenga majengo ya kisasa ya taasisi zake, bado kuna changamoto ya kupotea kwa baadhi ya nyaraka za Serikali kupitia taasisi hizo, hasa zinapohama kutoka jengo moja kwenda jengo jengine. Hali kama hii bila ya shaka yoyote imejitokeza kwa jengo la Mambo Msiige ambalo sasa limejengwa Hoteli ya ‘Park Hyatt’ na hatimae kuhamia katika jengo jipya la Sheria ‘House’ liliopo Mazizini.

(a) Je, Wizara yako imechukua hatua gani kudhibiti kupotea kwa nyaraka za taasisi zilizokuwepo katika jengo lililokuwa la Mambo Msiige.

(b) Je, kuna mkakati gani wa kuyahifadhi mafaili kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mfumo wa kompyuta, ili kuepusha athari mbali mbali zitakazopelekea kupoteza kumbukumbu muhimu za wananchi.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

178. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa hoja nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zimetokana na kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha za umma.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kuondoa changamoto hii.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

69. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na utamaduni wa wafanyabiashara wa embe na ndizi kuzitia moshi wa moto ili ziive haraka, na wakati mwengine hata hayo mazao bado hayajakomaa vizuri.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu jambo hili.

(b) Je, Mhe. Waziri, unawaeleza nini wafanyabiashara hao juu ya tabia hii.

167. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kuhakikisha kilimo kinaimarika nchini, kuna umuhimu mkubwa sana wa wakulima wetu kutumia mbolea ya asili isiyo na kemikali katika kilimo hicho na elimu ya matumizi bora ya mbolea hiyo ikatolewa kwa wakulima wetu.

(a) Kwa kiasi gani Wizara yako inatoa elimu juu ya matumizi ya mbolea ya asili kwa wakulima wetu.

(b) Ni asilimia ngapi ya wakulima wetu wanatumia mbolea ya asili isiyo na kemikali zozote.

(c) Ni upi mpango wa Serikali wa kugawa mbolea za asili zisizokuwa na kemikali zozote kwa wakulima wetu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

213. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Imekuwa jambo la kawaida kwa wamiliki wa meli kuwatoza abiria wanaosafiri kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam ada za mizigo melini bila ya kuzingatia masharti yaliyomo kwenye tiketi ikiwemo uzito anaoruhusiwa abiria kusafiri nao bila ya kuulipia, jambo ambalo limekuwa likileta usumbufu.

(a) Je, ni ipi ada halali ya meli ya kumlipisha abiria anayesafiri na mzigo kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam.

(b) Je, ni kiwango gani cha mzigo ambacho abiria anayesafiri kati ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam anaruhusiwa bila ya kukilipia melini.

(c) Je, ni utaratibu upi Serikali inautambua na imeutumia kupata kodi zinazotokana na ada za mizigo ya abiria melini kwa kipindi cha 2020 – 2023 na kiasi gani cha fedha Serikali imeingiza kwa kipindi hicho.

**Wizara ya Afya:**

174. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ugonjwa wa moyo ni miongoni mwa magonjwa yanayoongezeka kwa kasi hapa Zanzibar na athari zake ni kubwa kwa wananchi wetu.

Je, ni ipi takwimu ya ongezeko la tatizo la ugonjwa wa moyo hapa Zanzibar.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

188. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wakati wa zoezi la mitihani ya darasa la saba mwaka 2022, Serikali ilitumia baadhi ya gari za watu binafsi kusaidia harakati za mitihani hiyo. Hata hivyo, hadi leo Serikali haikutimiza makubaliano ya kuazimwa kwa gari hizo.

(a) Je, hadi sasa, Serikali inadaiwa kiasi gani na wamiliki wa gari hizo zilizotumika katika shughuli hiyo.

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea hadi leo hii wahusika hao kutokulipwa haki yao hiyo na lini watalipwa.

(c) Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kuhakikisha kwamba suala la mitihani linachukuliwa katika unyeti wake na halidharauliwi kama ilivyo sasa.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

169. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:


Wananchi wengi wamekuwa wakipata sintofahamu ya ukweli halisi wa baadhi ya maelezo ya historia ya Zanzibar.

Je, kwa mujibu wa utafiti wa Serikali, ni ipi historia halisi ya uwepo wa Soko Kuu la Biashara ya Utumwa baina ya Mkunazini na Kelele "Square" kwa maelezo yanayojitosheleza, ili wananchi wasipotoshwe kuelewa historia ya nchi yao.

## IV. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Kuweka Masharti Yanayohusika na Huduma za Miundombinu ya Tehama na mambo mengine yanayohusiana na hayo – Kusoma kwa mara ya Pili



Zanzibar,
22 Juni, 2023.

(Abdalla Ali Shauri)
Kny. <u>KATIBU WA BARAZA</u>